# KANUNI ZA UCHAGUZI ZA CHAMA

THTU

2022

## KANUNI ZA UCHAGUZI ZA CHAMA

Kanuni hizi zimetungwa chini ya ibara ya 115 (2) ya Katiba ya Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimuya Juu Tanzania toleo la Mwaka 2020.

### 1.0 KANUNI ZA UCHAGUZI WA CHAMA

Kanuni za Uchaguzi za Chama ngazi za Tawi na Taifa zinafuata misingi ya Katiba ya Chama, Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini sura 366. Kanuni hizi zitazingatia kwa ukamilifu Haki za Mwanachama.

### 1.1 NGAZI ZA UCHAGUZI

1. Kutakuwa na ngazi mbili za uchaguzi ambazo ni:
   a) Uchaguzi wa viongozi ngazi ya Taifa
   b) Uchaguzi wa viongozi ngazi ya Tawi

### 1.2 MAELEKEZO YA UCHAGUZI

Uchaguzi utafanyika kila baada ya miaka mitano kumalizika tangu mwaka ambao viongozi waliopo madarakani walichaguliwa.

Maelekezo ya awali ya uchaguzi yatakuwa kama ifuatavyo:

a) Katibu mkuu wa Chama atatangaza tarehe ya kuanza kupokea maombi ya kuwania nafasi mbalimbali za uongozi wa Chama ndani ya siku 14 baada ya baraza kuu kuidhinisha Tume ya uchaguzi.

b) Tume itatoa notisi ya uchaguzi itakayoeleza:
   (i) Tarehe ya wagombea kuchukua fomu.
   (ii) Tarehe ya kurudisha fomu kama ilivyotangazwa awali na Katibu Mkuu wa Chama.
   (iii) Tarehe ya kutangaza wagombea waliopitishwa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi wa Chama.
   (iv) Tarehe ya kuanza kampeni za uchaguzi.

(v) Tarehe ya uchaguzi.

c) Kamati ya uchaguzi itaandaa notisi ya uchaguzi wa viongozi wa tawi miezi miwili kabla ya Mkutano wa uchaguzi. Notisi hii itaelezea taarifa kama zilivyoainishwa katika ngazi ya Taifa.

d) Fomu za uchaguzi ngazi ya tawi zitarejeshwa kwa katibu wa kamati ya uchaguzi.

## 1.3 FOMU ZA UCHAGUZI

a) Kila mwanachama anayeomba nafasi ya uongozi atatakiwa kujaza fomu maalumu kama zilivyoainishwa kwenye jedwali la fomu katika kanuni hizi.

b) Fomu za kugombea uongozi zitatolewa Tume/Kamati ya Uchaguzi.

c) Muda wa kuchukua na kurudisha fomu utakuwa kama ilivyoainishwa katika notisi ya maelekezo ya uchaguzi.

d) Baada ya fomu kujazwa zitarudishwa kwa Katibu Mkuu wa Chama ikiambatana na uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi.

e) Fomu za uchaguzi ngazi ya tawi zitarudishwa kwa Katibu wa Kamati ya Uchaguzi.

f) Iwapo fomu itatumwa kwa njia ya posta tarehe iliyopo kwenye muhuri wa posta itahesabiwa kuwa ndiyo tarehe ya kuwasilisha fomu kwa Katibu Mkuu.

g) Fomu za kugombea uongozi katika ngazi ya tawi zitatolewa bure na Kamati ya Uchaguzi.

h) Endapo hakutakuwa na mgombea aliyejitokeza kuwania nafasi yoyote hadi kufika siku ya uchaguzi, Kamati ya Uchaguzi itaruhusu wagombea kuwasilisha maombi au kupendekezwa na wanaChama waliohudhuria kikao cha uchaguzi.

Fomu hazitapokelewa baada ya muda wa kurudisha fomu kumalizika.

## 1.4 IDADI YA FOMU ZA UCHAGUZI

Idadi ya fomu zitakazojazwa itategemea ngazi ya uchaguzi

a) Katika ngazi ya tawi zitajazwa nakala mbili za fomu:

i) Nakala moja itabaki kwa Katibu wa Kamati ya Uchaguzi.

ii) Nakala ya pili atabaki nayo mwombaji

b) Ngazi ya taifa zitajazwa nakala tatu (3) za fomu:

i) Nakala moja itabaki kwa katibu wa Tume ya uchaguzi.
ii) Nakala ya pili atabaki nayo mwombaji.
iii) Nakala ya tatu itatumwa kwenye tawi analotoka mwombaji.

### 1.5 UTUNZAJI WA ORODHA YA WAGOMBEA

Katibu wa Kamati ya Uchaguzi au Tume ataandaa shajara yenye orodha ya wagombea.

### 1.6 KADI ZA UTAMBULISHO

a) Kila Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Uchaguzi atapewa kadi ya utambulisho

b) Katibu Mkuu wa Chama ataandaa kadi hizo na kuzigawa kwa Wajumbe baada ya kuwasili kwenye eneo la Mkutano Mkuu wa uchaguzi.

### 1.7 NAFASI ZA UONGOZI

#### 1.7.1 Ngazi ya Taifa

Nafasi za Uongozi wa kuchaguliwa kwa ngazi ya Taifa zitakuwa kama ifuatavyo:

i) Mwenyekiti wa Chama.
ii) Mratibu Mkuu wa Kamati ya Wanawake.
iii) Mratibu Msaidizi wa Kamati ya Wanawake.
iv) Mweka Hazina wa Chama.
v) Mwakilishi wa Vijana.
vi) Mwakilishi wa WanaChama wenye Ulemavu.

#### 1.7.1 Ngazi ya Tawi

Nafasi za Uongozi wa kuchaguliwa kwa ngazi ya Tawi zitakuwa kama ifuatavyo:

i) Mwenyekiti wa Tawi.
ii) Katibu.
iii) Mweka hazina.
iv) Mratibu Mkuu wa Kamati ya Wanawake.
v) Mratibu Msaidizi wa Kamati la Wanawake.
vi) Mwakilishi wa WanaChama wenye Ulemavu.
vii) Mwakilishi/ Wawakilishi watakaochaguliwa kuwa wajumbe wa Halmashauri ya Tawi.
viii) Mwakilishi/Wawakilishi wa Tawi katika Mkutano Mkuu wa Chama Taifa.

## 1.8 SIFA ZA WAGOMBEA KWA NAFASI ZA UONGOZI WA CHAMA.

Sifa za wagombea wa nafasi za uongozi zitakuwa kama ifuatavyo: -

a) Awe mwanachama hai wa THTU kwa kipindi cha mwaka mmoja mfululizo na kuendeleaisipokuwa kwa matawi mapya.
b) Ngazi ya Taifa awe amehudumu katika nafasi ya uongozi kwenye Chama kwa miaka mitatu au zaidi.
c) Ngazi ya Tawi awe mwanachama wa THTU kwa Tawi husika kwa muda usiopungua mwaka mmoja.
d) Awe na Elimu kuanzia kiwango cha shahada au zaidi.
e) Kwa wajumbe wa halmashauri ya Tawi, awe na elimu ya kidato cha nne au sifa linganifu na elimu ya kidato cha nne.
f) Awe mwadilifu, mwaminifu na mwenye sifa njema mbele ya jamii.
g) Hatakiwi kulipa michango kwa mkupuo.
h) Asiwe ametiwa hatiani na mahakama kwa tuhuma za rushwa, jinai na unyanyasaji kijinsia na mengine yanayofanana na hayo.
i) Asiwe na nafasi ya uongozi wa kisiasa.
j) Awe raia wa Tanzania.
k) Awe mfanyakazi wa Taasisi ya Elimu ya Juu Tanzania mwenye ajira ya kudumu au ajira ya mkataba usio chini ya miaka mitano (5) wakati wa kugombea.
l) Wakati wa kugombea awe na miaka zaidi ya 5 ya kuwa kazini kabla ya kustaafu.
m) Asiwe mwanachama wa Chama kingine cha Wafanyakazi.
n) Awe ana akili timamu.
o) Kwa nafasi ya Mwekahazina wa Chama Taifa awe na shahada ya uhasibu au kiwango cha elimu sawa na shahada ya uhasibu pamoja na CPA(T).

## 2.0 UUNDWAJI WA TUME NA KAMATI YA UCHAGUZI

a) Kutakuwepo na Tume ya Uchaguzi itakayoundwa na wajumbe watano ( 5) katika ngazi ya taifa. Tume hii itaundwa na Baraza Kuu la Chama mwaka mmoja kabla ya tarehe ya uchaguzi.

b) Kutakuwepo na Kamati ya Uchaguzi itakayoundwa na wajumbe watatu (3) katika ngazi ya Tawi. Kamati hii itaundwa na Mkutano Mkuu wa Tawi miezi miwili kabla ya tarehe ya uchaguzi.

c) Katika kufanya uteuzi wa wajumbe wa Tume na Kamati ya Uchaguzi, mamlaka za uteuzi zitazingatia uwiano wa jinsia.

## 2.1 KAZI ZA KAMATI NA TUME YA UCHAGUZI

Kamati/Tume ya uchaguzi itakuwa na kazi zifuatavyo.

1. Kuongoza zoezi zima la uchaguzi kulingana na katiba na kanuni za uchaguzi
2. Kutangaza tarehe za kuanza mchakato wa uchukuaji wa fomu, urejeshwaji wa fomu na kampeni za uchaguzi.
3. Kuhakikisha muda wa zoezi la kuanza uchaguzi unaheshimika.
4. Kuhakiki utoshelevu wa karatasi za kura kulingana na idadi ya wajumbe.
5. Kuhakikisha kuwa wagombea wanapewa nafasi sawa ya kujibu maswali.
6. Kuhakikisha kuwa wagombea wanapewa muda na nafasi sawa ya kujieleza.
7. Kuhakikisha uchaguzi ni wa huru na haki.
8. Kuteua wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi.
9. Kuhakikisha kuwa kila mgombea anakuwa na mwakilishi wake wakati wa kuhesabu kura.
10. Kuhakiki sifa za wagombea kabla ya kuanza kwa kampeni na kufanyika kwa uchaguzi.
11. Kuchagua wagombea wenye sifa na kuwaengua wasio na sifa katika kila nafasi.
12. kutangaza matokeo ya uchaguzi.
13. Kuwafanyia usaili wagombea.
14. Kuthibitisha sifa za mgombea kwa nafasi aliyoomba.

### 2.1.1 KAZI ZA MWENYEKITI WA TUME/KAMATI YA UCHAGUZI

a) Mwenyekiti atakuwa ndiye msimamizi mkuu wa uchaguzi,

b) Atashirikiana na wajumbe wote na kuhakikisha uchaguzi ni wa huru na haki.

c) Atakuwa msemaji mkuu wa Tume/Kamati ya uchaguzi.

### 2.1.2 KAZI ZA KATIBU WA TUME/KAMATI YA UCHAGUZI

a) Kuratibu mchakato wa uchaguzi kwa ngazi husika kwa kushirikiana na wajumbe wenzake.
b) Kuhakikisha wanaChama wanapata taarifa za upatikanaji wa fomu.
c) Kuhakiki fomu za wagombea kama zimekidhi vigezo kabla ya kuzipokea kwa ngazi ya tawi.
d) Kuhakiki orodha ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Uchaguzi iwapo ni sahihi kwa ngazi husika.
e) Kuhakikisha eneo la Mkutano lina mazingira rafiki kwa wajumbe wa Mkutano.
f) Kuhakikisha Kanuni za Uchaguzi zinazingatiwa na kutekelezwa.

### 2.1.3 KAZI ZA WAJUMBE WENGINE

a) Kugawa karatasi za kupigia kura.
b) Kukusanya karatasi na masanduku ya kura.
c) Kuhakikisha uhalali wa wajumbe waliomo ukumbini kwa ajili ya kazi ya kupiga kura.
d) Kuhakikisha wajumbe wamepata mahitaji muhimu katika zoezi la kupiga kura.
e) Kuwaelewesha wajumbe kuhusu taratibu za uchaguzi.
f) Kuhesabu kura zilizopigwa na kumkabithi matokeo Mwenyekiti wa uchaguzi.

## 3.0 UCHUKUAJI NA UREJESHWAJI WA FOMU ZA UCHAGUZI

Mchakato wa uchukuaji wa fomu na kuzirejesha utafanyika kwa utaratibu ufuatao:-

1. Fomu za uchaguzi zitapatikana kupitia:
    - Tume/Kamati ya Uchaguzi ya Chama.
    - Tovuti ya Chama.
2. Fomu zote za maombi zitarudishwa kwa Katibu Mkuu kwa ngazi ya Taifa na kwa Katibu Kamati ya Uchaguzi kwa ngazi ya Tawi.
3. Mgombea atakayerudisha fomu atatakiwa asaini kwenye kitabu maalumu kilichoandaliwa.

## 4.0 UDHAMINI TOKA KWENYE TAIFA/TAWI.

(a) Mgombea anatakiwa awe na wadhamini wasiopungua kumi na tano, watano kutoka kwenye tawi lake na kumi kutoka katika matawi ya Chama katika Taasisi nyingine Kwa ngazi ya Taifa.

(b) Kwa ngazi ya Tawi

(i) kwa matawi yenye wanachama 10-50 wadhamini 3

(ii) kwa matawi yenye wanachama 51 na zaidi wadhamini 5

(C) Mdhamini hatatakiwa kudhamini mgombea zaidi ya mmoja kwa nafasi husika.

## 5.0 MCHAKATO WA UCHAGUZI

Tume/Kamati ya Uchaguzi itachambua maombi ya wagombea na kupitisha majina ya wanaokidhi vigezo.

Wagombea waliokidhi vigezo watatakiwa kwenda kwenye usaili mbele ya Tume/Kamati ya uchaguzi.

a) Wagombea wote watapewa taarifa na Tume/Kamati ya uchaguzi juu ya matokeo ya usaili.

b) Wagombea waliopita kwenye usaili watafuata taratibu zinazoendelea kama ambavyo itaelekezwa na Tume/Kamati ya uchaguzi.

c) Ikiwa atajitokeza mgombea mmoja kwa nafasi ya uongozi, Tume/Kamati itafata taratibu zote kama ilivyo aianishwa kwenye kanuni hizi.

d) Mgombea atakaye patikana na kuthibitika katika vitendo vya rushwa, unyanyasaji wa kijinsia na makosa mengine yanayofanana na hayo hataruhusiwa kuendelea kugombea nafasi ya uongozi kwenye Chama.

e) Mgombea anaweza kujitoa kugombea nafasi ya uongozi kwa kuwasilisha maombi yake kwa maandishi kwa mamlaka ya uchaguzi siku kumi na nne (14) kabla ya kupiga kura kwa ngazi ya Taifa na siku saba (7) kwa ngazi ya Tawi.

f) Baada ya mchujo, majina ya wagombea waliopitishwa yatatangazwa kwa ajili ya kuanza kampeni.

g) Vifaa kwa ajili ya uchaguzi vitaandaliwa mapema kabla ya siku yauchaguzi.

## 5.1 KAMPENI

Kampeni zitaanza baada ya kutangazwa majina ya wagombea na zitafanyika hadi siku moja kabla ya kupiga kura.

a) Wagombea hawataruhusiwa kufanya kampeni siku ya Mkutano Mkuu wa uchaguzi.

b) Mgombea atakaethibitika kuchafua/wachafua wagombea wengine, kuwadhalilisha na kufanya hila wakati wa kampeni, atakuwa amekiuka kanuni za uchaguzi.

c) Mgombea hataruhusiwa kufanya kampeni zinazochafua Chama na akithibitika kufanya hivyo atakuwa amekiuka kanuni za uchaguzi.

d) Mgombea hataruhusiwa kubandika vipeperushi au mabango ndani ya mita mia mbili (200) toka eneo la uchaguzi.

e) Mgombea hataruhusiwa kuanza kampeni kabla ya muda wa kampeni za uchaguzi kuanza.

f) Mgombea hataruhusiwa wakati wa kampeni, kutafuta wanachama wapya, kukusanya wanachama/wajumbe na kuwanunulia chakula, vinywaji au kufanya jambo lolote linaloweza kutafsiriwa kuwa ni kampeni chafu.

g) Mgombea wa nafasi ya uongozi atapata muda wa kupiga kampeni za kuomba kuchaguliwa.

h) Muda wa kampeni kwa uchaguzi ngazi ya Taifa utakua siku 21 na siku 14 kwa ngazi ya Tawi.

Mgombea atakaye kiuka Kanuni za Uchaguzi ataondolewa kuwa mgombea wa nafasi yoyote katika uchaguzi husika.

## 5.2 WAJUMBE HALALI

Wajumbe halali wa Mkutano wa Uchaguzi watakuwa: -

1. Wajumbe wote waliolipa ADA ya uanachama kwa mujibu wa Katiba ya Chama.
2. Matawi ambayo hayapeleki michango ya asilimia hamsini kwenda Chama Taifa

yatapoteza sifa na uhalali wa kupeleka wajumbe katika Mkutano Mkuu wa Uchaguzi Taifa.

3. Wajumbe wa Kamati/Tume ya uchaguzi watakuwa wajumbe wa Mkutano wa uchaguzi na hawataruhusiwa kupiga kura.
4. Akidi ya kikao cha uchaguzi itakuwa theluthi mbili ya wajumbe halali wa kikao cha uchaguzi.
5. Wajumbe watahakiki akidi kwa kuhesabu namba zao kwa sauti.

## 6.0 UPIGAJI KURA

Mchakato wa kupiga kura kwenye Uchaguzi Mkuu utakuwa kama ifuatavyo: -

a) Kabla ya zoezi la upigaji kura kuanza, kila mgombea atapewa dakika tatu za kujieleza.
b) Mgombea ataulizwa maswali yasiozidi matatu na atajibu yote kwa muda usiozidi dakika 5.
c) Mjumbe atapiga kura kwa kuweka alama ya vema ndani ya kisanduku kilicho mbele ya jina la mgombea anayemchagua.
d) Ikiwa nafasi ya mgombea ina jina moja, wajumbe watapiga kura kwa kuweka alama ya vema kwenye kisanduku cha NDIO au HAPANA.
e) Upigaji wa kura utakuwa ni wa siri na kura moja kwa mgombea mmoja.
f) Kura ya siri itapigwa hata kama mgombea ni mmoja kwenye nafasi iliyoombwa.
g) Mshindi wa nafasi ya Mwenyekiti Taifa atatakiwa kupata zaidi ya nusu ya kura za wajumbe wa Mkutano wa uchaguzi.
h) Mshindi wa nafasi ya Mwenyekiti/ katibu wa tawi atatakiwa kupata zaidi ya nusu ya kura za wajumbe wa Mkutano wa uchaguzi.
i) Washindi wa nafasi nyingine zote za uongozi watatokana na wingi wa kura zitakazopigwa.

## 6.1 VIONGOZI WALIOKUWA MADARAKANI

a) Siku ya Mkutano Mkuu wa uchaguzi, viongozi waliokuwa madarakani watatakiwa kujiuzulu nafasi za uongozi. Mwenyekiti wa ngazi husika atatoa tamko la kujiuzulu kwa niaba ya viongozi wengine.
b) Viongozi waliojiuzulu kwa ngazi ya tawi wataendelea kuwa wajumbe halali na watakua na haki ya kupiga kura.
c) Viongozi waliojiuzulu kwa ngazi ya Taifa watahudhuria kwenye Mkutano wa Uchaguzi kama waalikwa isipokuwa hawatakuwa na haki ya kupiga kura.

## 6.2 KARATASI ZA KURA

a) Kila nafasi itakayogombewa itakuwa na karatasi husika ya kura.
b) Baada ya wagombea kujieleza karatasi za kura zitagawiwa.
c) Kwa kila nafasi ya uongozi, karatasi za kura zitaonesha majina kamili ya wagombeayakiwa yameorodheshwa kwa alfabeti kwa kutumia majina ya ukoo.

## 6.3 KUHESABU KURA NA MATOKEO

Utaratibu wa kuhesabu kura na matokeo utakuwa kama ifuatavyo:-

1. Kila mgombea wa nafasi yoyote ya uongozi atachagua wakala mmoja kushuhudia zoezila kupiga kura.

2. Mwenyekiti wa Kamati/Tume ya Uchaguzi atasaidiana na wasaidizi wake pamoja na mawakala wa kila mgombea katika kuhesabu kura.

3. Karatasi ambazo zilitumika kupiga kura zitahifadhiwa na Kamati/Tume ya Uchaguzi kwa kipindi cha mwaka mmoja.

4. Matokeo ya kura yataorodheshwa kwenye fomu maalum na msimamizi wa uchaguzi,mgombea na wakala wake watatakiwa kusaini fomu hiyo.

## 6.4 KUTANGAZA MATOKEO

a) Mwenyekiti wa Kamati/Tume ya uchaguzi atatangaza matokeo ya uchaguzi mbele ya wajumbe wa kikao.

b) Mwenyekiti wa Kamati/Tume ya uchaguzi ataanza kutangaza matokeo kwa utaratibu ufatao:
    i) Idadi ya kura zilizopigwa.
    ii) Kura zilizoharibika.
    iii) Kura halali.

c) Atatangaza kura alizopata kila mgombea kwa kuanza na mwenye kura chache zaidi hadi mwenye kura nyingi zaidi.

d) Mwisho atamtangaza mshindi.

e) Kwa nafasi ya mgombea yenye jina moja endapo atapata kura zaidi ya nusu za hapana atahesabika kuwa ameshindwa na nafasi hiyo itabaki wazi hadi hapo itakapojazwa mujibu wa Katiba.

f) Mshindi atatakiwa kupewa cheti maalumu cha ushindi.

g) Washindi watatakiwa kuapishwa.
    (i) Kwa ngazi ya Taifa na mwanasheria wa Chama katika kikao cha kamati kuu ambacho kitakuwa maalum.
    (ii) Kwa ngazi ya Tawi na mwanachama ambaye ni wakili au wakili yoyote katika kikao cha halmashauri ya tawi la chama ambacho kitakuwa maalum.

h) Baada ya matokeo kutangazwa mwenyekiti aliyechaguliwa atapewa nafasi ya kushukuru wajumbe kwa niaba ya wenzake.

## 7.0 RUFAA

a) Kutakuwa na kamati ya rufaa katika ngazi mbili.
    (i) Kamati ya rufaa ya uchaguzi ngazi ya Tawi.
    (ii) Kamati ya rufaa ya uchaguzi ngazi ya Taifa.

b) Kamati ya rufaa ya uchaguzi ngazi ya Tawi itateuliwa na mkutano mkuu wa tawi. Kikao cha mkutano mkuu wa wanachama tawi kitateua wajumbe watatu miongoni mwao watakaounda kamati ya rufaa ya uchaguzi. Endapo mazingira yataruhusu mkutano mkuu wa tawi unaweza kuteua wajumbe wa kamati ya rufaa kutoka matawi ya chama yaliyo jirani.

c) Kamati ya rufaa ya uchaguzi ngazi ya Taifa itakuwa na wajumbe watatu ambao wataidhinishwa na mkutano mkuu wa chama Taifa kabla ya uchaguzi.

d) Wajumbe watatu wa kamati ya rufaa ya uchaguzi ngazi ya Taifa watapendekezwa na kamati kuu ambao majina yao yaatapelekwa Baraza kuu kwa ajili ya kupitishwa na baadae mkutano mkuu kwa ajili ya kuidhinishwa.

e) Mwenyekiti atatakiwa kuwa ni mwanachama mwenye taaluma ya sheria.

f) Wajumbe wa Kamati hii hawatatokana na wajumbe wa Mkutano Mkuu wala Baraza Kuu la Chama.

g) Maamuzi ya Kamati ya rufaa yatakuwa ya mwisho.

h) Tume/Kamati ya rufaa itahudumu ndani ya mwaka mmoja toka tarehe ya kuundwa kwake.

## 7.1 MCHAKATO WA KUKATA RUFAA

a) Mgombea asiyeridhika na matokeo ya uchaguzi atajaza Fomu ya rufaa na kuiwasilisha kwa mamlaka husika ndani ya siku kumi na nne (14) kwa ngazi ya Taifa na ndani ya masaa 48 kwa ngazi ya tawi toka siku ya uchaguzi.

b) Rufaa itakayowasilishwa nje ya muda haitapokelewa.

c) Rufaa itatakiwa ionyeshe pamoja na mambo mengine jinsi katiba ya Chama na kanuni za uchaguzi zilivyokiukwa au kuvunjwa.

d) Rufaa zitasikilizwa na kutolewa maamuzi ndani ya siku thelasini (30) toka siku ya kuwasilishwa rufaa.

e) Mrufani atalipa ada ya kiasi cha shilingi elfu hamsini (Ths. 50,000/=) kwa ngazi ya Taifa na elfu ishirini (Tsh. 20,000/=) kwa ngazi ya tawi kabla ya kuwasilisha rufaa yake.

f) Mrufani atatakiwa kuambatanisha risiti ya malipo pamoja na fomu za rufaa wakati wa kuwasilisha.

g) Chombo pekee cha kubatilisha matokeo ni chenye mamlaka ya kusikiliza rufaa katika ngazi husika.

## 8.0 TAHADHARI YA UCHAGUZI

a) Mgombea yoyote atakayethibitika kuvunja kifungu chochote cha Katiba au Kanuni hizi hataruhusiwa kuendelea na uchaguzi na kama ameshakwisha

kuchaguliwa atanyang’anywa ushindi alioupata na hataruhusiwa kugombea uongozi THTU kwa kipindi cha miaka mitano.

b) Ikithibitika kuwa mjumbe wa Kamati/Tume ya uchaguzi anafanya upendeleo kwa mgombea mmoja wapo, atavuliwa ujumbe.

**CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA**
S.L.P **35928 DAR ES SALAAM, TANZANIA**
Simu: **+255 22 2401581**, Nukushi: **+255 22 2401582**
Tovuti: www.thtu.or.tz, Barua Pepe: thtuhq@thtu.or.tz

**FOMU YA MAOMBI YA MWENYEKITI WA CHAMA WA TAIFA TF:1A**

(*ijazwe na mgombea)*

Jina la Mwombaji: ____________________________Jinsia:

Elimu:____________________Simu:_____________Barua pepe:__________

Mwajiri:_____________________________Idara:___________________

Masharti ya Ajira: (*Kudumu/mkataba)*

Mkoa:________________Tawi:______________________

Saini ya Mwombaji:____________Tarehe:_______________

WADHAMINI

| NA. | MAJINA | TAASISI ANAYOTOKA | TAREHE | SAINI |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

Mimi mtajwa hapo juu kwa hiari yangu mwenyewe nimeamua kuomba uongozi ili niweze kutumia uwezo wangu kushirikiana na wanachama wenzangu katika kulinda na kutetea haki na maslahi yangu, ya wanachama wenzangu na wafanyakazi wote.

Jina:____________________________________Saini:______________Tarehe:______________

Fomu imepokelewa leo tarehe ………………………………..

Jina ……………………………………………….. Saini……………………………….

Maoni ya Tume ya Uchaguzi ya Taifa

________________________________________________________________________________
________________________________________________________________________________
________________________________________________________________________________
________________________________________________________________________________
________________________________________________________________________________

Jina ……………………………………………….. Saini…………………

| | |
|---|---|
| THTU | **CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA**<br>S.L.P **35928 DAR ES SALAAM, TANZANIA**<br>Simu: **+255 22 2401581**, Nukushi: **+255 22 2401582**<br>Tovuti: www.thtu.or.tz, Barua Pepe: thtuhq@thtu.or.tz |

**FOMU YA MAOMBI YA NAFASI YA MRATIBU MKUU/MSAIDIZI WA KAMATI YA WANAWAKE TAIFA TF:1B**

*(ijazwe na mgombea)*

Jina la Mwombaji: ______________________________Jinsia:

Elimu:______________________Simu:______________Barua pepe:___________

Mwajiri:_______________________________Idara:_____________________

Masharti ya Ajira: (*Kudumu/mkataba)*

Mkoa:__________________Tawi:________________________

Saini ya Mwombaji:______________Tarehe:________________

WADHAMINI

| NA. | MAJINA | TAASISI ANAYOTOKA | TAREHE | SAINI |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

Mimi mtajwa hapo juu kwa hiari yangu mwenyewe nimeamua kuomba uongozi ili niweze kutumia uwezo wangu kushirikiana na wanachama wenzangu katika kulinda na kutetea haki na maslahi yangu, ya wanachama wenzangu na wafanyakazi wote.

Jina:_______________________________________Saini:_______________tarehe:_______________

Fomu imepokelewa leo tarehe …………………………………….

Jina ……………………………………………….. Saini……………………………………

Maoni ya Tume ya Uchaguzi ya Taifa

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

Jina ……………………………………………….. Saini…………………

**CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA**
S.L.P **35928 DAR ES SALAAM, TANZANIA**
Simu: **+255 22 2401581**, Nukushi: **+255 22 2401582**
Tovuti: www.thtu.or.tz, Barua Pepe: thtuhq@thtu.or.tz

**FOMU YA MAOMBI YA NAFASI YA MWEKA HAZINA WA CHAMA TAIFA TF:1C**

*(ijazwe na mgombea)*

Jina la Mwombaji: ______________________________Jinsia:

Elimu:______________________Simu:______________Barua pepe:___________

Mwajiri:_______________________________Idara:_____________________

Masharti ya Ajira: (*Kudumu/mkataba)*

Mkoa:__________________Tawi:________________________

Saini ya Mwombaji:______________Tarehe:________________

WADHAMINI

| NA. | MAJINA | TAASISI ANAYOTOKA | TAREHE | SAINI |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

Mimi mtajwa hapo juu kwa hiari yangu mwenyewe nimeamua kuomba uongozi ili niweze kutumia uwezo wangu kushirikiana na wanachama wenzangu katika kulinda na kutetea haki na maslahi yangu, ya wanachama wenzangu na wafanyakazi wote.

Jina:___________________________________Saini:______________Tarehe:______________

Fomu imepokelewa leo Tarehe …………………………………..

Jina ……………………………………………….. Saini…………………………………

Maoni ya Tume ya Uchaguzi ya Taifa

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

Jina ……………………………………………….. Saini…………………

**CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA**
S.L.P **35928 DAR ES SALAAM, TANZANIA**
Simu: **+255 22 2401581**, Nukushi: **+255 22 2401582**
Tovuti: www.thtu.or.tz, Barua Pepe: thtuhq@thtu.or.tz

**FOMU YA MAOMBI YA MWAKILISHI WA VIJANA WA CHAMA TAIFA TF:1D**

(*ijazwe na mgombea)*

Jina la Mwombaji ______________________________Jinsia:

Elimu:_____________________Simu:_____________Barua pepe:__________

Mwajiri:______________________________Idara_____________________

Masharti ya ajira: (*Kudumu/mkataba)*

Mkoa:_________________Tawi:________________________

Saini ya Mwombaji:_____________Tarehe:________________

WADHAMINI

| NA. | MAJINA | TAASISI ANAYOTOKA | TAREHE | SAINI |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

Mimi mtajwa hapo juu kwa hiari yangu mwenyewe nimeamua kuomba uongozi ili niweze kutumia uwezo wangu kushirikiana na wanachama wenzangu katika kulinda na kutetea haki na maslahi yangu, ya wanachama wenzangu na wafanyakazi wote.

Jina:_____________________________________Saini:______________Tarehe:______________

Fomu imepokelewa leo tarehe …………………………………

Jina ……………………………………………….. Saini…………………………………

Maoni ya Tume ya Uchaguzi ya Taifa

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

Jina ……………………………………………….. Saini…………………

**CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA**
S.L.P **35928 DAR ES SALAAM, TANZANIA**
Simu: **+255 22 2401581**, Nukushi: **+255 22 2401582**
Tovuti: www.thtu.or.tz, Barua Pepe: thtuhq@thtu.or.tz

**FOMU YA MAOMBI YA MWAKILISHI WA WANACHAMA WENYE ULEMAVU TAIFA TF:1E**

*(ijazwe na mgombea)*

Jina la Mwombaji: ______________________________Jinsia:

Elimu:______________________Simu:______________Barua pepe:___________

Mwajiri:_______________________________Idara:_____________________

Masharti ya Ajira: (*Kudumu/mkataba)*

Mkoa:__________________Tawi:________________________

Saini ya Mwombaji:______________Tarehe:________________

WADHAMINI

| NA. | MAJINA | TAASISI ANAYOTOKA | TAREHE | SAINI |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

Mimi mtajwa hapo juu kwa hiari yangu mwenyewe nimeamua kuomba uongozi ili niweze kutumia uwezo wangu kushirikiana na wanachama wenzangu katika kulinda na kutetea haki na maslahi yangu, ya wanachama wenzangu na wafanyakazi wote.

Jina:____________________________________Saini:______________Tarehe:______________

Fomu imepokelewa leo Tarehe ………………………………….

Jina ……………………………………………….. Saini…………………………………

Maoni ya Tume ya Uchaguzi ya Taifa

________________________________________________________________________________
________________________________________________________________________________
________________________________________________________________________________
________________________________________________________________________________
________________________________________________________________________________

Jina ……………………………………………….. Saini…………………

**CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA**
S.L.P **35928 DAR ES SALAAM, TANZANIA**
Simu: **+255 22 2401581**, Nukushi: **+255 22 2401582**
Tovuti: www.thtu.or.tz, Barua Pepe: thtuhq@thtu.or.tz

**FOMU YA KUOMBA KUWA MGOMBEA WA NAFASI YA UONGOZI THTU TAWI TF:2A**

*(ijazwe na mgombea)*

Jina la Mwombaji: ______________________________Jinsia:

Elimu:______________________Simu:______________Barua pepe:___________

Mwajiri:_______________________________Idara:_____________________

Masharti ya Ajira: (*Kudumu/mkataba)*

Mkoa:__________________Tawi:________________________

Saini ya Mwombaji:______________Tarehe:________________

## NAFASI ZA UONGOZI NGAZI YA TAWI

| NA. | NAFASI | ALAMA YA VEMA KWA NAFASI HUSIKA | SAINI |
|---|---|---|---|
| 1. | Mwenyekiti. | | |
| 2. | Katibu. | | |
| 3. | Mweka Hazina | | |
| 4. | Mratibu Mkuu wa Wanawake. | | |
| 5. | Mratibu Msaidizi wa Wanawake. | | |
| 6. | Mwakilishi wa wafanyakazi wenye ulemavu | | |
| 7. | Mwakilishi wa kuchaguliwa na wanachama kuwa mjumbe wa halmashauri(kutegemea na idadi ya wanachama) | | |
| 8. | Mwakilishi wa Tawi katika Mkutano Mkuu wa Chama Taifa (kutegemea na idadi ya wanachama) | | |
| 9. | Mjumbe kamati ya wanawake | | |

**WADHAMINI**

| NA. | MAJINA | TAASISI ANAYOTOKA | TAREHE | SAINI |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

Mimi mtajwa hapo juu kwa hiari yangu mwenyewe nimeamua kuomba uongozi ili niweze kutumia uwezo wangu kushirikiana na wanachama wenzangu katika kulinda na kutetea haki na maslahi yangu, ya wanachama wenzangu na wafanyakazi wote.

Jina:____________________________________Saini:______________tarehe:______________

Fomu imepokelewa leo tarehe ……………………………….

Jina ……………………………………………….. Saini……………………………….

Maoni ya Kamati ya Uchaguzi.

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

Jina ……………………………………………….. Saini…………………

**CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA**
S.L.P **35928 DAR ES SALAAM, TANZANIA**
Simu: **+255 22 2401581**, Nukushi: **+255 22 2401582**
Tovuti: www.thtu.or.tz, Barua Pepe: thtuhq@thtu.or.tz

**FOMU YA MATOKEO YA UCHAGUZI MKUU WA THTU TAIFA TF:3A**

**NAFASI YA UONGOZI**:___________________

| **NA.** | **MAELEZO** | **JUMLA YA KURA** |
|---|---|---|
| | Idadi ya wapiga kura | |
| | Jumla ya kura zilizopigwa | |
| | Kura zilizoharibika | |
| | Kura halali | |
| | **Jina la Mgombea** | |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |
| 8. | | |
| 9. | | |
| 10. | | |

Mwenyekiti wa Tume/Kamati ya uchaguzi

Saini:___________________Tarehe:_________________

**CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA**
S.L.P **35928 DAR ES SALAAM, TANZANIA**
Simu: **+255 22 2401581**, Nukushi: **+255 22 2401582**
Tovuti: www.thtu.or.tz, Barua Pepe: thtuhq@thtu.or.tz

**FOMU YA KUHESABU KURA TF:3B**

| S/N | JINA LA MGOMBEA | KURA ALIZOPATA | SAHIHI YA MDHAMINI |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |
| 5 | | | |
| 7 | | | |
| 8 | | | |
| 9 | | | |
| 10 | | | |

Imetolewa na Kamati/Tume ya Uchaguzi

Jina la Msimamizi: ______________________

Cheo:__________________________________

Sahihi:__________________________________

Tarehe:__________________________________

Muhuri:___________________________________

**CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA**
S.L.P **35928 DAR ES SALAAM, TANZANIA**
Simu: **+255 22 2401581**, Nukushi: **+255 22 2401582**
Tovuti: www.thtu.or.tz, Barua Pepe: thtuhq@thtu.or.tz

## FOMU YA KUPIGA KURA TF:3C

| PICHA | JINA | ALAMA YA VEMA (√ ) |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |

**FOMU YA RUFAA KWA NAFASI MBALIMBALI ZA UONGOZI WA CHAMA**

**TF:4A**

***(ijazwe na mkata rufaa)***

Jina la Mrufani: ______________________________

Simu:_____________Barua pepe:_________________

Nafasi alilyogombea:___________________________

Tawi:________________________

Mkoa:___________________________

Kifungu cha Katiba/Kanuni za Chama Kilichovunjwa:-

i)

ii)

iii)

Sababu za ziada za rufaa:

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

Viambatanisho/Ushahidi kuwasilishwa wakati wa kurejesha fomu hii.

Saini ya Mrufani________________________Tarehe ______________________

Imepokelewa

Saini:________________________________Tarehe:________________

Katibu wa Tume/Kamati ya uchaguzi